

KATIBA INITIATIVE

MAPENDEKEZO YA WAFUGAJI KWENYE KATIBA MPYA

MAPENDEKEZO YA WAFUGAJI KWENYE KATIBA MPYA

1. UTANGULIZI

"*Tumetenga, kwa mfano, maeneo maalum kwa ajili ya mazao kama pamba, kahawa, tumbaku na katani lakini hatujatenga maeneo kama hayo kwa ajili ya mifugo. Tumetenga hata maeneo maalum kwa ajili ya pundamilia (hifadhi za taifa) lakini wafugaji wananing'inia hewani tu."*

-Mwalimu J.K. Nyerere, Morogoro, 1981.

1.1. Historia ya wafugaji na wawindaji/wakusanya matunda wa asili Tanzania.

1.2. Wafugaji wa asili ni jamii ya watanzania waishio kwa kutegemea mifugo yao ya asili katika nyanda za malisho na hujipatia takriban mahitaji yao yote kutokana na mifugo. Mifugo hiyo hutegemea malisho ya nyasi, chumvichumvi na upatikanaji wa maji. Hata hivyo ili kulinda mazingira, kufikia malisho ya mifugo yao, maji, kukwepa magonjwa ya mifugo na kuruhusu nyanda hizo za malisho kuzalisha malisho mapya mara nyingine wafugaji hulazimka kuhama kutoka katika uwanda mmoja wa malisho kwenda katika uwanda mwingine. Hivyo basi, uhamaji wa wafugaji una tija kwa sababu wafugaji wa asili hutumia eneo moja la kiekologia kwa misimu tofauti na hatimaye kurudi katika eneo la awali kwa kutegemeana na uwepo wa malisho, chumvi, maji na kutokuwepo na magonjwa ya mifugo. Mara nyingi watunga sera wameonekana kutoelewa tija hii.

Kutokana na mfumo wao wa kiekologia kukumbwa na changamoto na kutokana na wafugaji kuondolewa katika maeneo yao ya asili ya malisho, ulazima huo wao wa kuhama umekua mkubwa mno kwa siku za karibuni. Wafugaji wa asili wamejikuta wakihamia katika maeneo yasiyokuwa ya kwao kiasili na hivyo kukumbana na jamii zingine ambazo sio za kifugaji jambo na hivyo kuzuka kwa migogoro ya matumizi ya ardhi ikihusisha wenyeji wanaowakuta katika maeneo hayo. Hivi sasa wafugaji wa asili wameenea Mikoa ya Arusha, Morogoro, Manyara, Mwanza, Shinyanga, Singida, Mbeya, Tanga, Tabora na Dodoma.

1.3. **Wawindaji/wakusanya matunda wa asili** huishi kwa kutegemea uwindaji wa asili, ukusanyaji wa matunda mwitu, majani na mizizi mwitu na urinaji wa asali. Kitakwimu, Wawindaji/wakusanya Matunda ni machache sana katika jamii ya watanzania. Jamii hizi hujumuisha Wahadzabe na Waakie. Wahadzabe huishi katika wilaya za Karatu, Mbulu, Manyoni na Meatu. Waakie kwa upande wao huishi katika wilaya ya Kiteto.

1.4. Takwimu zinaonyesha kwamba ufugaji wa asili unaajiri takriban watu 5,000,000; sawa na 10% ya idadi ya watanzania wote. Pia unachangia 97% ya mifugo yote nchini na kuwapatia 98% ya Watanzania nyama na maziwa. Mifugo ya ufugaji wa asili pia inachangia 30% ya uzalishaji wa sekta ya kilimo na 18% pato ghafi la taifa.

Hata hivyo, mitizamo hasi juu ya umuhimu wa namna hizi za uzalishaji katika taifa la Tanzania ni changamoto kubwa inayoikabili jamii hizi za Wafugaji na wawindaji/wakusanya matunda wa asili tangu wakati wa ukoloni hadi sasa. Kwa vile mfumo wa kimila wa ufugaji haukushabihiana na mfumo wa kikoloni wa umilikaji ardhi, wakoloni hawakuwekeza katika sekta za mifugo na uwindaji wa asili. Sababu nyingine ni kwamba maeneo yaliyokaliwa na wafugaji na wawindaji/wakusanya matunda wa asili yalikua ni maeneo yaliyo mbali na huduma za usafirishaji. Sera na sheria za kikoloni zilitungwa bila kujali uwepo wa wafugaji wa asili pamoja na wawindaji/wakusanya matunda wa asili.

Tangu baada ya uhuru, serikali za awamu tofauti tofauti zimetunga sera na sheria zinazolenga kutokomeza mifumo ya maisha ya jamii hizi za asili. Hivyo basi, Sera na sheria nyingi nchini ikiwemo Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 hazitetei jamii hizi na mifumo yao ya uzalishaji wa asili kama ilivyo kwa jamii zingine za Tanzania kama vile wakulima. Wafugaji na wawindaji/wakusanya matunda wapo kwenye sekta isiyo rasmi na wamekuwa wakipuuzwa na kutopewa nafasi ya kujiendeleza.

1.5. Ufugaji wa asili ni moja kati ya njia kuu za uchumi na matumizi ya ardhi Tanzania. Inakadiriwa kuwa kati ya hekta milioni 88 za eneo lote la ardhi la nchi, hekta milioni 60 ni maeneo ya nyanda za malisho. Hivyo, ni dhahiri kuwa sehemu kubwa ya ardhi ya Tanzania inafaa kwa ufugaji kuliko shughuli nyingine ya kiuchumi. Maeneo mazuri ya ufugaji yamesaidia nchi kuwa na mifugo mingi na kushika nafasi ya tatu kwa idadi ya mifugo barani Afrika. Tanzania inakadiriwa kuwa na zaidi ya ng'ombe milioni 21

ambao kati yao, asilimia 98 ni ng'ombe wa asili wanaotunzwa na jamii mbalimbali nchini. Idadi kubwa ya mifugo ya asili inachangiwa pamoja na mambo mengine, uwezo wake wa kustahimili mazingira magumu na yaliyo kame ambayo ndiyo sehemu kubwa ya nchi yetu.

1.6. Sekta ya mifugo inachangia asilimia nne (4%) kwenye pato la Taifa. Inakadiriwa kwamba, kama sehemu ya kilimo, mifugo huchangia asilimia 30 ya pato lote la kilimo. Hata hivyo, ufugaji ungeweza kuwa na mchango mkubwa zaidi kwenye pato la Taifa endapo sekta hiyo ingepata uwekezaji stahili. Kwamba, sekta hiyo imekuwa na uwekezaji mdogo sana tangu enzi za ukoloni ikilinganishwa na maeneo mengine ya kiuchumi kama vile kilimo cha mazao. Nchi kama Botswana ambayo ina mifugo michache kuliko Tanzania, imeweza kuwekeza ipasavyo katika ufugaji na hatimaye imefanikiwa kuongeza uchangiaji wa sekta hiyo katika pato lake la Taifa.

1.7. Mbali na kuchangia katika pato la Taifa, ufugaji wa asili unafaida nyingine zikiwemo, vyanzo vya mapato, uhakika wa chakula na ajira. Kwa ujumla inakadiriwa zaidi ya **asilimia 10** ya watanzania wanategemea sana ufugaji wa asili kwa ajili ya kuendesha maisha yao ya kawaida. Aidha, ufugaji unasaidia kuendeleza sekta ya kilimo kwa vile ni chanzo muhimu cha mbolea na wanyama kazi wanaotumika katika kulima na usafirishaji wa mazao.

1.8. Pamoja na nafasi kubwa ya ufugaji wa asili katika maendeleo ya Taifa, mitizamo ya kisera imekua hasi kwa kiasi kikubwa tangu enzi za ukoloni. Wafugaji wa asili wanaonekana kuwa watu wakorofi wanaohamahama ovyo na kuingilia haki za watumiaji wengine wa ardhi. Aidha, ufugaji wa asili huonekana kama njia ya kizamani (primitive) ya kujipatia kipato na mara nyingi mchango wake katika pato la Taifa unaonekana hafifu. Vilevile, ufugaji wa asili unaonekana kuwa chanzo kikubwa cha uharibifu wa mazingira na mmomonyoko wa udongo. Kadhalika, mifugo ya asili huonekana ni ya kizamani na isiyokuwa na tija ikilinganishwa na aina nyingine ya mifugo. Pia, jinsi wafugaji wanavyomiliki na kutumia ardhi inaonekana kuwa siyo kwa njia sahihi na haifai katika mwendelezo wa nyanda za malisho.

1.9. Mitizamo hasi kuhusu ufugaji wa asili, imesababisha kutungwa sera na sheria ambazo kwa kiasi kikubwa zimewanyima wafugaji haki kama Watanzania wengine. Sehemu kubwa ya ardhi ya wafugaji imegeuzwa kuwa ya matumizi mengine yanayoonekana kuwa na tija zaidi. Sehemu kubwa ya ardhi ya hifadhi nchini mwetu ni ardhi ambazo zilikuwa za

wafugaji. Hifadhi za wanyamapori kama **Ngorongoro**, **Serengeti**, **Manyara**, **Tarangire**, **Mkomazi**, **Arusha**, **Tarangire, Maswa**, n.k zilikuwa ni maeneo ya wafugaji yaliyoamuliwa kuwa hifadhi za wanyamapori. Mbali na uhifadhi, ardhi za wafugaji zimechukuliwa vilevile kwa ajili ya mashamba makubwa ya kilimo kama yale ya Basuto Hanang, West Kilimanjaro, Sukenya Loliondo na mashamba makubwa yaliyopo Wilayani Simanjiro, n.k. Maeneo mengine makubwa yamechukuliwa kwa ajili ya kambi za jeshi (kama Monduli) na ujenzi wa viwanja vya ndege (kama Arusha na Kilimanjaro).

1.10. Kuchukuliwa kwa ardhi za wafugaji kumeleta athari mbaya si kwa wao tu lakini vilevile kwa Watanzania wengine. Uhamaji wa Wafugaji kutoka katika maeneo yao asili (mikoa ya kaskazini, kanda ya ziwa na mikoa ya kati) kuelekea mikoa mingine (mikoa ya kusini, pwani na magharibi) kumesababisha migogoro mikubwa na jamii zingine na hivyo kuendelea kutishia amani ya nchi.

1.11. Kutokana basi na maelezo ya hapo juu kuhusu hali ya wafugaji wa asili, sisi Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Vikundi vya Wafugaji tulioanzisha Mtandao wa Wafugaji Kuhusu Katiba (**Katiba Initiative**), tunaleta mapendekezo yafuatayo kwenye Tume ya Katiba. Tuna imani kubwa kuwa **Katiba Mpya** ni fursa ya kipekee ya kushughulikiwa changamoto mbalimbali zinazowakabili wafugaji wa asili.

2. MSINGI WA KULETA MAPENDEKEZO MBELE YA TUME

2.1. Ufugaji wa kiasili ni njia ya maisha na ya kiuchumi inayotegemewa na watanzania walio wengi (zaidi ya asilimia kumi), hivyo si mfumo wa kubeza. Mitizamo hasi ya kisera na kisheria imedidimiza mfumo huu na kusababisha changamoto na matatizo mengine yanayohitaji utatuzi wa haraka. Katiba mpya ndio fursa ya kuuangalia mfumo huu upya na kutatua changamoto zilizopo ili uendelee kuchangia katika uchumi wa Taifa na jamii husika.

2.2. Migogoro ya Ardhi kati ya wafugaji na wamiliki wengine wa ardhi (wakulima, wawekezaji, serikali) imeongezeka siku za karibuni hivyo kuhatarisha amani ya nchi. Amani na utulivu katika nchi yetu vitaimarishwa tu pale migogoro hii itakapotafutiwa suluhu ya kudumu. Katiba mpya ni fursa ya kipekee ya kutatua migogoro hii.

2.3. Wafugaji wamepoteza ardhi zao kwa wingi tangu wakati wa ukoloni kupisha matumizi yanayoonekana kuwa na manufaa zaidi (hifadhi, kilimo, miji n.k). Katiba mpya ni fursa muhimu ya kurudisha ardhi hizo au pale itakaposhindikana kufanya hivyo basi zilipwe fidia au uwepo msaada wa kisheria wa kusaidia jamii za wafugaji wa kiasili. Jambo la muhimu zaidi tunalopenda kusisitiza ni kwamba, Katiba Mpya iwe nafasi ya kipekee ya kuweka ulinzi wa uhakika wa ardhi za wafugaji na wazalishaji wengine wadogo wadogo.

2.4. Moja ya njia ambazo wafugaji hupoteza Sana ardhi zao za malisho ni kwa njia ya Uhifadhi WA Wanyamapori; Serikali kwa nyakati tofauti tofauti imetwaa ardhi za jamii hizi na kuzigeuza kuwa hifadhi za taifa za wanyamapori. Utwaaji huu wa ardhi kwa uhifadhi ulianza tangu wakati wa utawala wa kikoloni. Kwa mfano hifadhi ya taifa ya Serengeti ilianzishwa na Serikali ya kikoloni wa Uingereza mwaka 1958. Wakoloni waliwaondoa kwa nguvu watu *Bila fidia wala ardhi mbadala* kwa namna ya kikatili kwa kuchoma makazi yao, kuwapiga na kuwaweka baadhi yao vizuizini. Hivi ndivyo wakoloni walivyowafukuza wa-Maasai kwenda Mashariki mwa hifadhi; ya Serengeti yaani Loliondo na Ngorongoro. Wa-Sukuma, wa-Taturu, wa-Nata, wa-Ikoma, wa-Ngoreme, wa-Kuria, wa-Jaluo na makabila mengine yalifukuzwa kwenda Magharibi mwa hifadhi ya Serengeti. Leo hii wakati Serengeti ina ukubwa wa kilomita za mraba 14,763; karibu sawa na nchi ya Ubelgiji, wafugaji wa asili wanazidi kusukumwa pembezoni na hata wakati wa ukame hawaruhusiwi kuingia pembezoni mwa hifadhi kunusuru mifugo yao.

Mwaka 1961, wakati Tanganyika inapata uhuru, kulikuwa na hifadhi moja tu ya taifa; yaani Hifadhi ya Taifa ya Serengeti. Leo hii hifadhi za Taifa zimeongezeka hadi kufikia 15. Serikali ina jitihada za makusudi ya kuongeza maeneo haya kwa:

- Kuanzisha maeneo mapya ya hifadhi ama
- Kuongeza ukubwa wa hifadhi zilizopo. Wahanga wa jitihada hizi za serikali wamekuwa wafugaji ambao wameendelea kupoteza maeneo yao ya asili.

Kwa mfano, mwaka 1987 Serikali kwa mara ya kwanza iliagiza kuondolewa wafugaji kutoka kwenye iliyokuwa Pori tengefu la Mkomazi. Mwaka 1988 Idara ya Wanyamapori iliwaondoa kwa nguvu wafugaji 1754 kwa kuchoma makazi yao na kuwachapa viboko. Wafugaji walipoteza ardhi yenye ukubwa wa kilomita za mraba 3,234; au ekari 808,000.

Wafugaji walitumia mkondo wa mahakama kwa madai waliondolewa kinyume na sheria. Mahakama ya rufaani ilitoa haki kwa wafugaji wachache waliotoa ushahidi mahakamani. Badala ya Kuamuru wafugaji warudishwe katika maeneo yao, Mahakama iliagiza Wafugaji hao wachache walipwe fidia na kupewa ardhi mbadala. Hata hivyo hadi leo hawajaipata ardhi hiyo mbadala. Kwa maana hiyo hata vyombo vya mahakama vimekua vikishindwa kuwapatia Wafugaji haki juu ya ardhi yao inayoondoka.

Mfano mwingine ni upanuzi wa hifadhi za Taifa kwa kumeza ardhi za vijiji: Mwaka 2008 Serikali iliongeza ukubwa wa Hifadhi ya Ziwa Manyara kutoka kilomita za mraba 330 hadi kilomita za mraba 649 na hivyo kuathiri kwa kiasi kikubwa shughuli za ufugaji. Mbali na Ziwa Manyara, Hifadhi ya Taifa ya Tarangire inahamisha mipaka na kumeza ardhi ya Kijiji cha Kimotorok Wilaya ya Simanjiro na vijiji vingi. Vijiji vinavyopakana na maeneo ya hifadhi takriban nchi nzima hususan hifadhi za taifa za Kilimanjaro, Saadani, Udzungwa, Kitulo, Mikumi, Arusha, Ruaha na Katavi vinaendelea kulalamika.na kupaza kilio hicho hicho cha ardhi kutwaliwa. Vijiji ambavyo bado havijaathirika havina uhakika wa ardhi yao kwa siku za usoni kutokana na wimbi hili.

Serikali bado inaongeza eneo la hifadhi ya taifa ya Serengeti pamoja na hifadhi hiyo kuwa na ukubwa wa kilomita za mraba 14,763; karibu sawa na nchi ya Ubelgiji ilihali ardhi ya ufugaji ikiendelea kusinyaa. Hali hii inatishia kuzuka kwa migogoro mikubwa ya ardhi kutokana na Serikali kuhamisha mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti. Kwa mfano mwezi Desemba mwaka 2012 wanakijiji wa Kijiji cha Ololosokwan walidaiwa kung'oa bikon ambazo hifadhi ya Serengeti imesimika kinyemela kwenye ardhi ya kijiji chao kinyume cha sheria na bila kukipa kijiji taarifa.

Hivi karibuni, Serikali pia iliongeza Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kutoka kilomita za mraba 10,300 za awali hadi kufikia kilomita za mraba 20,226. Na tarehe 15 Desemba 2008 Rais Jakaya Mrisho Kikwete alitia saini tangazo la Serikali kuridhia upanuzi huo. Wahanga wakubwa wa zoezi hili ni wafugaji waliohamishwa kwa nguvu na bila kifidiwa ama kupewa ardhi mbadala.

2.5. Ufugaji wa asili ni rasilimali yenye tija sana kwa maendeleo ya Taifa kama jitihada za makusudi zikichukuliwa kuuendeleza. Tanzania ina mifugo

mingi sana (ya tatu Barani Afrika) lakini mchango wake katika pato la Taifa si mkubwa sana ikilinganisha na nchi zenye mifugo michache zaidi kama Botswana na Kenya. Hivyo, ulinzi wa kikatiba utasaidia kufungua fursa za kuuendeleza ufugaji kwa maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

2.6. Kumekuwepo na ukiukwaji mkubwa wa haki za wafugaji tangu zamani mpaka siku za karibuni unaotokana pamoja na mambo mengine, kuondolewa/kufukuzwa kwa mabavu kwa wafugaji hao kutoka katika ardhi zao kwa ajili ya kupisha uwekezaji au kwa madai ya kuzuia uharibifu wa mazingiria. Kuanzia mwaka 2006 kumekuwepo na ongezeko la unyanyasi na kufukuzwa kwa wafugaji katika maeneo mbalimbali nchini bila kufuata taratibu za kisheria. Mifano mizuri ni kufukuzwa kwa wafugaji katika **Bonde la Ihefu** (2006), **Loliondo** (2009), **Kilosa** (2008), **Kilombero na Ulanga** (2012), **Vilima Vitatu-Manyara** (2010) n.k. Mara nyingine kufukuzwa huku kumeendana na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu na serikali inaonyesha kutochukua hatua zozote dhidi ya unyanyasaji na ukatili huo. Licha ya kwamba Tume mbalimbali ziliundwa kuchunguza uvunjifu wa haki za binadamu katika matukio hayo, mapendekezo ya tume hizo hayajafanyiwa kazi na serikali kama ilivyotarajiwa. Mathalan, Tume ya **Jaji Othman Chande** iliundwa kuchunguza unyanyasaji wa kutisha wakati wa kuondolewa kwa wafugaji kutoka Bonde la Ihefu, Wilayani Mbarali. Tume hiyo ilifanya kazi yake lakini cha kushangaza tangu mwaka 2006 hadi leo mwaka 2013, ripoti ya tume hiyo haijawekwa wazi, mapendekezo yake hayafahamiki na haijulikani endapo yametekelezwa au yatatekelezwa kama yalivyopendekezwa kutokana na uchunguzi uliofanyika. Kwa msingi huo, tunaona kuwa, Katiba mpya ni fursa ya kipekee ya kutoa nafasi kwa wafugaji walioonewa kudai fidia na zaidi ya hapo nchi iwe na mifumo dhabiti ya kisheria ya kuhakikisha kuwa matukio kama haya hayatokei tena.

2.7. Suala lingine la kuzingatia ni ongezeko la idadi ya watu pamoja na mifugo ikilinganishwa na ukubwa wa ardhi uliopo. Kwamba, kasi ya ongezeko la watu na mifugo inahitaji mipango madhubuti ya matumizi ya Ardhi kitaifa. Ufinyu wa ardhi pamoja na mabadiliko ya tabia nchi kwa pamoja vinatoa changamoto zinazohitaji uvumbuzi wa haraka. Mipango ya namna ya kukabiliana na changamoto hizi itawezekana tu kwa utaratibu wa katiba na hasa pale ufugaji wa asili ukitambuliwa na katiba kama njia ya matumizi ya ardhi inayohitaji kutengewa maeneo maalum katika mpango wa matumizi ya ardhi wa kitaifa.

3. MAPENDEKEZO YA MSINGI

3.1. MAPENDEKEZO YA KIUJUMLA

3.1.1. Katiba Mpya itamke wazi na kulinda mifumo yote ya kiuchumi inayotegemewa na Watanzania, ikiwa ni pamoja na kilimo, **ufugaji wa asili**, **uwindaji wa asili, uvuvi,** n.k. Kumekuwa na desturi ya kusema Tanzania ni nchi ya wakulima na wafanyakazi na hivyo kujenga taswira potofu kuwa mifumo mingine ya kiuchumi haina nafasi katika maendeleo ya Taifa. Tunatoa pendekezo hili kwa sababu kutambuliwa kwa aina fulani ya mfumo wa kiuchumi ndio mwanzo wa kuwekewa vipaumbele katika maendeleo ya Taifa.

3.1.2. Katiba mpya itambue na kutaja **ufugaji wa asili kama njia halali ya kiuchumi katika matumizi ya ardhi.** Hili ni muhimu kutokana na mtizamo wa sasa (unaoakisiwa na sheria, sera na mipango ya maendeleo ya Taifa) ambao unaonyesha kuwa ufugaji wa asili siyo mfumo sahihi na wenye tija katika matumizi ya ardhi. Kwamba, mitizamo hiyo imesababisha kuwepo kwa uwekezaji mdogo katika sekta ya mifugo na hatimaye kuathiri mchango wa sekta hiyo katika pato la Taifa.

3.1.3. Makundi mbalimbali na Mifumo yao ya Uzalishaji; Imefika wakati sasa serikali kutambua uwepo wa makundi maalum na ya pembezoni nchini kwetu. Utambuzi huo wa jamii ya pembezoni (marginalized communities) unapaswa uwe wa sheria iliyotungwa na bunge kwamba jamii hii ambayo kutokana na udogo wake au kwa sababu nyingine yoyote haikuweza kushiriki kikamilifu katika mfumo mkuu wa kijamii na kiuchumi au jamii ya kiasili ambayo kwa sababu ya mahitaji na matamanio yake imeendelea kubaki tofauti na watanzania wengine. Ili kutambua makundi haya maalum na pembezoni, tunapendekeza yafuatayo;

3.1.3.1. Serikali itambue kwamba uwepo wa umoja wa kitaifa unajengwa na misingi ya uwepo wa jamii mbalimbali zilizotofautiana katika namna ya kupata mahitaji yao huku zikiwa na imani, mila, desturi na mifumo tofauti ya uzalishaji mali; haina budi, katiba mpya ikatambua umoja wa kitaifa na utofauti wa jamii mbalimbali zinazounda taifa hilo. (Fostering national unity by recognizing diversity). Kwa msingi serikali itambue uwepo wa

makundi ambayo kutokana na sababu mbalimbali za kihistoria wamekua pembezoni na wanahitaji ulinzi, wa kikatiba wao kama jamii, na mifumo yao ya umiliki wa ardhi na rasilimali zingine.

3.2. MAPENDEKEZO YANAYOHUSU MASUALA YA ARDHI PEKEE

3.2.1. Katiba Mpya iwe na sura inayojitegemea yenye kuzungumzia Ardhi na rasilimali zingine za Taifa (wanyapori, madini, misitu, maji, mazingira, mafuta, gesi n.k.). Misingi mikuu ya namna ya kusimamia rasilimali hizi ni vizuri ikawepo kwenye katiba ili kutoa kinga isiweze kubadilishwa kirahisi kama ilivyo katika sheria za kawaida zinazotungwa na Bunge. Katika utaratibu wa Katiba ya sasa, rasilimali hizi zimekuwa zikitungiwa sheria kulingana na maslahi ya wachache wakiwemo wawekezaji.

3.2.2. Katiba mpya iweke utaratibu wa kutenga maeneo maalum kwa ajili ya ufugaji wa asili. Hatua hii ni muhimu kama njia mojawapo ya kutafutia suluhu migogoro mbalimbali iliyopo kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa Ardhi. Namna ya kufanya hivi ina changamoto zake lakini inawezekana kwani tayari kuna maeneo ambayo yanafahamika kama maeneo ya wafugaji (ikiwemo mikoa ya Arusha, Manyara, Singida, Shinyanga, Simiyu, Mara, n.k.). Vilevile, mikoa/maeneo ambayo siyo maeneo ya wafugaji wa asili, bado inawezakana kutenga maeneo maalum ya wafugaji. Lengo hili litafikiwa pale tu Katiba Mpya itakapokuwa na utaratibu wa mpango wa matumizi ya Ardhi wa Kitaifa. Maeneo yatakayotengwa kwa ajili ya ufugaji wa asili yatungiwe sheria ya namna ya kusimamiwa na kuendelezwa.

3.2.3. Kutengwa kwa ardhi maalum ya wafugaji iendane sambamba na kuruhusu wafugaji kuhama kutoka sehemu moja hadi nyingine ndani ya maoneo yao ya asili na yale yatakayotengwa kwa ajili yao kwa utaratibu utakaowekwa na Katiba Mpya. Hili linaweza kufanyika kwa kuainisha njia za mapito ya mifugo (stock routes) ambazo zitatungiwa sheria ya namna ya kuendesha. Hili liende sambamba na kufunguliwa kwa njia za zamani za mapito ya mifugo ambayo imefungwa na hifadhi za wanyama pori na mashamba makubwa.

3.2.4. Katiba mpya ianzishe aina mpya ya ardhi itakayoitwa **ardhi za jamii** (community lands). Sheria za Ardhi za sasa zinatambua ardhi za vijiji, ardhi ya jumla na ardhi ya hifadhi. Utaratibu wa sasa hautoi kinga dhidi ya matumizi au ugawaji wa maeneo na ardhi yenye umuhimu wa

kipekee kwa ajili ya matumizi ya jamii au vikundi maalum. Mfano mzuri ni kilima cha 'Endoinyo Ormoruak' kilichopo Hai mkoani Kilimanjaro ambacho hutumiwa na Wamasai wote Tanzania na Kenya kufanyia matambiko wakati wa sherehe kubwa za Wamasai kutoka kwenye kundi la vijana na kuwa wazee. Eneo hili kwa sasa limevamiwa na mashamba kutokana na kukosekana kwa uangalizi katika mfumo wa sasa wa sheria za ardhi. Hivyo, kuna haja ya katiba mpya kuanzisha ardhi ya jamii ambayo itakuwa ni ardhi inayokaliwa, kutumika na kusimamiwa na jamii au kikundi cha watu kwa ajili ya shughuli za kuabudu, kuzikia, ufugaji, uwindaji, n.k. Usimamizi wa ardhi hizi usimamiwe na jamii au kikundi husika kwa mujibu wa sheria za kimila au kidini za jamii au kikundi hicho.

3.2.5. Katiba mpya itambue **miliki ya pamoja ya ardhi** (communal/collective ownership of land) kwa wafugaji na jamii zingine inayoratibiwa na taasisi za jadi kwa mujibu wa sheria za mila za jamii mbalimbali. Kufanya hivi ni muhimu kwa sababu wafugaji wanamiliki na kutumia ardhi na rasilimali zingine za malisho kwa pamoja. Utaratibu wa sasa wa kisheria wa kugawa ardhi na kumilikisha ardhi kwa mtu mmoja mmoja kunahatarisha uwepo wa ufugaji wa asili. Katika utaratibu wa sasa wafugaji wanamiliki maeneo yao kwa pamoja bila kuwa na uhakika na kinga ya kisheria.

Kukosekana kwa miliki inayotambuliwa kisheria kumesababisha ardhi nyingi za wafugaji kuchukuliwa na watu wengine kwani huonekana tupu na isiyokaliwa.

3.2.6. Katiba mpya itambue haki ya wafugaji kuruhusiwa **kuingia na kulisha mifugo ndani ya Hifadhi za wanyama na misitu** nyakati za ukame. Ingawa kuna changamoto za utekelezaji wa jambo hili, tunapendekeza itungwe sheria maalum ya namna ya kuratibu uingiaji wa wafugaji wakati wa ukame hasa pale inapoonekana kuwa kufanya hivyo hakutakuwa na athari za kimazingira na kwa wanyama pori. Suala hili linawezekana kwani inafahamika kuwa katika baadhi ya maeneo ya wafugaji, mifugo inachanganyika na wanyama pori bila madhara yoyote. Mfano wa mchanganyiko huo ni maeneo wanakoishi wafugaji wa Kimasai wenye mila kali dhidi ya kuwinda au kula nyama za wanyamapori. Katika ukanda wa Afrika Mashariki, tayari hili linafanyika kwenye mazingira ya hifadhi za Taifa kama zilizopo Tanzania. Sera ya Taifa ya Ardhi ya Kenya ya mwaka (2009) inaeleza kuwa:

183. *To secure pastoralists livelihoods and tenure to land, the Government shall:*

(a) Recognize pastoralism as a legitimate land use and production system

(b).....

(f) ***Provide for flexible and negotiated cross boundary access to protected areas, water, pastures and salt licks among different stakeholders for mutual benefit...***

3.2.7. Katiba mpya iweke usimamizi wa Ardhi na Rasilimali zingine za Taifa katika vyombo vya kiwakilishi/kidemokrasia badala ya utaratibu wa sasa wa kuweka ardhi mikononi mwa Rais, vyombo na serikali za vijiji. Katika hili tunapendekeza yafuatayo:

1. Iundwe **Tume ya Taifa ya Ardhi** (National Land Commission) itakayokuwa na jukumu la kusimamia Ardhi yote ya Taifa. Tunapendekeza Tume iwe na wajumbe wasiozidi kumi watakaoteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muuungano wa Tanzania kwa sharti la majina hayo yajadiliwe na hatimaye kupitishwa na Bunge. Wajumbe wa Tume ya Ardhi watakuwepo madarakani kwa miaka mitano lakini wanaweza kuchaguliwa kwa kipindi kingine kimoja cha miaka mitano. Wajumbe hao wapatikane kwa kuzingatia masuala ya jinsia, makundi mbalimbali ya uzalishaji, taaluma, ukanda, n.k

2. Katika ngazi ya kijiji tunapendekeza katiba itamke kuwa **Mkutano Mkuu wa kijiji** ndio chombo kinachosimamia ardhi za vijiji tofauti na utaratibu wa sasa unaoweka usimamizi huo upo mikononi mwa kikundi kidogo cha hadi watu 25 kwenye Halmashauri ya kijiji. Kuwekwa usimamizi wa ardhi mikononi mwa watu wachache katika utaratibu wa sasa kumesababisha watu hao kutumia madaraka vibaya kwa kutoa ardhi za vijiji bila ridhaa ya wanavijiji husika.

3.2.8. Katiba mpya itamke **kiwango cha juu** cha umiliki wa ardhi nchini Tanzania (maximum land holding size) kwa mtu mmoja mmoja. Tunapendekeza ufanyike utafiti na tathmini kuhusu mahitaji ya Ardhi

kwa ajili ya matumizi mbalimbali ili kuweza kuamua kiwango cha umiliki wa Ardhi kwa matumizi tofauti.

3.2.9. Katiba iainishe kwa ufasaha maana ya **maslahi ya umma** (public interest) katika Ardhi. Ni muhimu kufanya hivyo kwa sababu kukosekana kwa tafsiri na maana iliyo wazi ya 'maslahi ya umma' kumesababisha ardhi za jamii kuchukuliwa na serikali kwa kisingizio cha kuwa na maslahi ya umma. Aidha, sheria zilizopo za ardhi zinachukuliwa kuwa 'maslahi ya umma' ni pamoja na uwekezaji. Tafsiri hiyo ni potofu kwa sababu mara nyingine kutolewa ardhi kwa wawekezaji kunaweza kusiwe kwa ajili ya 'maslahi ya umma' bali ni kwa ajili ya maslahi ya wawekezaji hao na wazawa wachache ndani ya nchi.

3.2.10. Katiba mpya itambue na kutolea **ufumbuzi uonevu wa kihistoria (historical injustices)** katika ardhi. Uonevu/manyanyaso ya kihistoria katika ardhi yanaweza kumaanisha uporaji wa Ardhi uliofanywa dhidi ya jamii fulani au kikundi cha watu bila kufuata taratibu za sheria katika kipindi cha nyuma tangu enzi za ukoloni. Kutokana na uporaji huo, jamii hizi zimeachwa zikiwa zinatangatanga au kutokuwa na uhakika wa maisha katika maeneo wanamoishi kwa sasa. Kwa hili tunaweza tukatoa mifano halisi:

Mfano wa kwanza: Kuondoshwa Wamasai katika hifadhi ya Serengeti:

Mfano mzuri wa uonevu ya kihistoria ni pale wafugaji wa Kimaasai walipoondolewa kwa mabavu kwenye ardhi yao ya asili pale ilipoanzishwa hifadhi ya Taifa ya Serengeti mwaka 1958/59. Katika kile kinachodaiwa ni makubaliano na serikali ya kikoloni ya waingereza, Wamasai waliruhusiwa kuendesha maisha yao ya ufugaji ndani ya hifadhi ya Ngorongoro. Hata hivyo, Wamasai hao hawajatimiziwa ahadi za makubaliano husika kwani eneo la Hifadhi ya Ngorongoro limeendelea kuendeshwa kwa maslahi ya uhifadhi na utalii zaidi kuliko maendeleo ya wafugaji kama ilivyokubaliwa.

Mfano wa pili: Kutimuliwa kwa Watatoga Hanang

Mfano mwingine mzuri wa manyanyaso hayo ni pale sehemu kubwa ya kabila la Kitatoga walipoondolewa kimabavu kwenye ardhi yao ya asili wilayani Hanang mkoani Manyara kupisha kilimo cha mashamba makubwa ya Ngano miaka ya 1970. Wakati wa uporaji huu hakuna fidia yeyote iliyolipwa au ardhi mbadala iliyotolewa kwa Watatoga na hivyo kufanya kabila zima kuwa wakimbizi katika nchi yao.

Kutokana na makosa hayo ya kihistoria tunapendekeza katiba mpya ije na utaratibu wa kutolea suluhu manyanyaso hayo kama ifuatavyo:

1. Katiba mpya itamke wazi kuwa kuna haja ya kuyatafutia ufumbuzi manyanyaso hayo ikiwa ni pamoja na kueleza bayana (meaning and scope) maana ya manyanyaso hayo kihistoria.

2. Katiba itoe utaratibu wa watu walioonewa au wenye madai ya halali ya uonevu huu kuweza kupeleka malalamiko mbele ya vyombo husika kwa ajili kupata fidia au nafuu nyingine ya kisheria.

3. Tunapendekeza kazi ya kupokea, kuchuja na kutolea maamuzi malalamiko ya kihistoria ifanywe na Tume ya Taifa ya Ardhi.

4. Katiba mpya iweke utaratibu wa kuitaka Serikali kupitia upya sheria zilizotungwa kwa ajili ya kuhalalisha uonevu huo, ili zifanyiwe marekebisho stahiki. Mfano wa sheria hizo ni kama sheria ya Hifadhi ya Ngorongoro ya mwaka 1959 inayoendelea kuwakandamiza wafugaji na kuwanyima fursa za maendeleo na haki za msingi kama watanzania wengine.

5. MAPENDEKEZO YANAYOHUSU RASLIMALI ZA ASILI NA MAZINGIRA PEKEE

5.1. Katiba mpya iweke **usimamizi wa raslimali za wanyamapori** mikononi mwa jamii zinazoishi ndani au mipakani mwa maeneo ya wanyamapori. Hatua hii ni muhimu kwa sababu hivi sasa rasilimali za wanyamapori zimewekwa chini ya usimamizi wa serikali na mashirika yake na hivyo kuwanyima wananchi fursa ya kusimamia

na kuwa sehemu ya maamuzi ya rasilimali zinazopatikana kwenye maeneo yao. Katika hili tunatoa mapendekezo yafuatayo:

1. **Hifadhi za Taifa** na maeneo mengine ya hifadhi za wanyamapori (hifadhi za akiba, mapori tengefu, n.k.) yawekwe moja kwa moja chini ya usimamizi wa Halmashauri za Wilaya zinazopakana na hifadhi husika. Katika hili tunaweza kujifunza kutoka kwa nchi jirani ya Kenya ambako hifadhi za wanyapori zinasimamiwa moja kwa moja na Halmashauri za Wilaya (County Councils).

2. Katiba iweke utaratibu wa kuhakikisha kuwa jamii zinazoishi ndani au jirani na maeneo ya wanyamapori **zinafaidika na mapato** yanayotokana na wanyamapori. Kwa hili tunapendekeza Katiba Mpya iweke utaratibu wa kuhakikisha kuwa jamii hizi zinapata kiasi kisichopungua **asilimia 50%** ya mapato yote yanayotokana na rasilimali za wanyamapori zilizopo kwenye maeneo yao.

5.2 Katiba mpya itamke wazi kuwa **ardhiza vijiji/jamii hazigeuzwi** kuwa hifadhi za wanyamapori bila kupata idhini ya vijiji zinazomiliki ardhi hizo. Pendekezo hili ni muhimu kwa sababu ardhi za wafugaji zimekuwa zikigeuzwa kuwa hifadhi za wanyamapori bila wao kukubali au kushirikishwa jambo ambalo limesababisha jamii hizo kupoteza ardhi na rasilimali zingine za malisho. Katika hili dhana ya wao kukubali kwa uhuru wao na huku wakijua maana ya wao kukubali **(Prior, Free and Informed Consent)** ni muhimu kama njia ya haki ya kutengeneza uhalali wa ardhi yao kugeuzwa kuwa maeneo ya hifadhi za wanyamapori.

5.3 Katiba mpya itambue na kulinda misitu ya jamii na vijiji, njia za jadi za kutumia na kumiliki vyanzo vya maji.

6. MAPENDEKEZO YANAYOHUSU MILA NA HAKI ZA MILIKI-BUNIFU (INTELLECTUAL PROPERTY RIGHTS)

6.1. Katiba mpya itambue na kulinda mila na tamaduni za jamii mbalimbali nchini kama chemichemi ya umoja wetu kama taifa na utofauti wetu kama jamii mbalimbali. Desturi na mila nyingine za

watanzania zinapotea kwa kasi ya ajabu kwa kukosa ulinzi wa kisera na kisheria.

6.2. Katiba mpya itambue na kulinda milikibunifu (intellectual property rights) za watu binafsi na jamii kwa ujumla ikiwa ni pamoja na kuweka taratibu za kisheria za kuhakikisha kuwa zinalindwa zisije kunakiliwa na kumilikiwa na watu wengine bila ruhusa maalum kwa mujibu wa sheria. Pendekezo hili ni muhimu kwa sababu milikibunifu nyingi za watanzania zimenakiliwa na kutumiwa na makampuni ya nje na kwa manufaa ya kibiashara bila idhini ya watanzania. Mfano mzuri ni kunakiliwa na kumilikiwa kwa chembechembe hai za kondoo aitwaye **Masai Red Sheep (Tanganyika Sheep)** na kampuni ya Australia bila idhini ya Wamasai au Watanzania ambao ndio hasa wamiliki halisi wa ubunifu huo.

6.3. Katiba mpya iweke utaratibu wa kutoa malipo na fidia kwa jamii ambazo milikibunifu zinatumika na watu wengine. Katika utaratibu wa sasa makampuni mengi ya nje yanajipatia faida kubwa kwa kuiba milikibunifu za watanzania bila ya wao kupata faida yoyote.

6.4. Tunapendekeza katiba mpya itamke wazi kuwa kila mtanzania awe na uhuru wa kutumia lugha na mila zake bila kuingiliwa na mtu mwingine. Pendekezo hili linatokana na ukweli kwamba**watanzania** wengi wanaendelea kuenzi na kushikilia mila zao ikiwa ni pamoja na lugha zao.

7. MAPENDEKEZO YANAYOHUSU SHERIA ZA MILA NA TAASISI ZA JADI

7.1. Katiba mpya itambue taasisi za jadi kama nguzo na chanzo muhimu cha hekima, mila na sheria za kimila. Taasisi za jadi(customary institutions) zimeendelea kufanya kazi na taasisi rasmi za kiserikali (formal institutions) bila taasisi hizo za kijadi kutambuliwa rasmi na sheria. Taasisi za jadi zimeendelea kuwa nguzo muhimu katika utatuzi wa migogoro, usimamizi wa ardhi na rasilimali zingine pamoja na kuwa chemichemi ya kuhifadhi mila na desturi za jamii mbalimbali.

7.2. Katiba mpya itoe fursa kwa taasisi za jadi kutolea maamuzi migogoro na masuala mengine yanayohusiana na mila kwa kutumia sheria za mila za jamii husika.

7.3. Ili kuwezesha taasisi za jadi ziweze kutambuliwa na kufanya kazi kwa mujibu wa sheria za nchi, tunapendekeza katiba mpya ianzishe utaratibu ufuatao:

1. Itambue rasmi kuwa taasisi za jadi ziwe sehemu rasmi ya mfumo wa serikali za mitaa. Katika hili wawakilishi wa taasisi za jadi wawe sehemu ya maamuzi katika vyombo vya maamuzi katika serikali za mitaa(serikali za vijiji, Halmashauri za wilaya, n.k). **AU;**

2. Taasisi za jadi ziweke utaratibu wa kufanya kazi sanjari (side by side) na taasisi rasmi. Kwa nguvu ya Katiba Mpya, sheria zitungwe ili kuweza kuainisha maeneo ambayo yatafanyiwa kazi na taasisi za mila. **AU;**

3. Kama haiwezekani kutambua kisheria taasisi za jadi katika nchi nzima, Katiba Mpya itambue na kuzipa nguvu taasisi za jadi za jamii ambazo bado zinatumia sana kazi/shughuli za taasisi hizi katika maisha ya kawaida. Jamii za kifugaji ni mfano mzuri wa jamii ambazo taasisi za jadi bado ni sehemu kubwa ya maisha yao ya kila siku. Kutambua na kuruhusu kuwepo kwa taasisi za jadi ni sehemu kubwa ya kuenzi na kulinda mila za kitanzania.

8. MAPENDEKEZO YANAYOHUSU MFUKO MAALUM WA KULETA USAWA WA MAENDELEO (EQUALISATION FUND)

8.1. Tunapendekeza Katiba Mpya ianzishe mfuko maalum kwa ajili ya kuleta usawa wa kimaendeleo nchini. Hii ni kutokana na ukweli usiopingika kuwa kuna mikoa, wilaya na jamii ambazo zipo nyuma kimaendeleo ikilinganishwa na maeneo mengine kutokana na sababu nyingi zikiwemo za kihistoria. Mfuko huu utatoa fursa ya kurekebisha tofauti hizi ambazo hazina tija kwa mustakabali wa nchi ya watu walio sawa. Fursa ya kutungwa katiba mpya itumike kuleta usawa miongoni mwa Watanzania wote. Katika kuhakikisha kuwa mfuko unaanzishwa tunapendekeza utaratibu ufuatao utumike:

1. Katiba itamke kuwa Serikali itatenga asilimia moja ya pato la Taifa kwa ajili ya mfuko huu.

2. Itungwe sheria maalum ya namna ya kuanzisha mfuko huu na namna ya kuuendesha ikiwa ni pamoja na namna na vigezo vya kutambua maeneo yaliyoachwa nyuma kimaendeleo.

3. Mfuko huu uundiwe Bodi Maalum ya kusimamia, ikiwa na baadhi ya wajumbe kutoka Mikoa, Wilaya au jamii ambazo zipo nyuma kimaendeleo.

4. Bajeti na matumizi ya fedha za mfuko huu iwe sharti kujadiliwa na kuidhinishwa na Bunge.

5. Matumizi ya Mfuko huu ni lazima yaelekezwe kwenye maeneo ya huduma muhimu za jamii kama elimu, afya, maji na barabara.

6. Mfuko huu unaweza kufutwa pale itakaponekana kuwa usawa wa kimaendeleo umepatikana katika nchi nzima.